**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents | Government Budget Speeches

1992-06-18

# Hotuba ya Waziri wa Fedha Mh. Kighoma Malima (Mb) akiwasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato ya Serikali kwa mwaka 1992-93

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/675

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

284

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Hotuba ya Waziri wa Fedha, Prof. Kighoma A. Malima (Mb), katika Bungetarehe 18 Juni, 1992, akiwasilisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 1992/93

1992

KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM — TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, PROF. KIGHOMA A. MALIMA (MB), KATIKA BUNGE TAREHE 18 JUNI, 1992, AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 1992/93

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili kujadili, na baadaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 1992/93.

2. Mheshimiwa Spika, mwanzoni kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki katika kukamilisha zoezi hili la Bajeti. Juhudi zao zimewezesha kuleta Bungeni mapendekezo ya Bajeti hii. Maandalizi ya Bajeti huwahusisha watu wengi na vyombo mbali mbali vya Taifa. Hivyo ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru Naibu Waziri wa Fedha, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na wafanyakazi wenzake, viongozi na wafanyakazi wa Tume ya Mipango, Wizara za sekta mbali mbali, Mikoa, Mashirika na Taasisi za Kitaifa, kwa mchango wao katika kukamilisha Bajeti hii. Aidha, ningependa kutoa shukrani za pekee kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa uchapishaji wa nyaraka mbalimbali na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kutayarisha Miswada ya Sheria Kazi hii isingekamilika bila ya mchango mkubwa uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Mathias Kihaule, Mbunge wa Ludewa, ambao wamekuwa wakichambua kwa undani mapendekezo ya Serikali ya Bajeti hii. Wote hao wanastahili pongezi kwa mchango wao.

3. Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha aliyenitangulia, Mheshimiwa Steven Kibona, naye anastahili pongezi na shukrani maalum. Kwani yeye ndiye aliyesimamia sehemu kubwa ya maandalizi ya bajeti hii. Kadhalika katika muda mfupi, unaozidi kidogo miaka miwili, ambao aliongoza Wizara ya Fedha, maamuzi mengi makubwa na ya msingi yametekelezwa, ikiwa ni pamoja na kuvunja ukiritimba wa Benki ya Taifa ya Biashara na kuanzisha ushindani katika sekta hii kutokana na kuruhusu kuanzishwa tena kwa benki binafsi, kufanya marekebisho ya sheria ya kudhibiti fedha za kigeni pamoja na kuweka taratibu za kurekebisha mashirika ya umma ili kuwezesha baadhi ya mashirika hayo kuimarishwa kifedha na kiuongozi, kuingia katika ubia, na yale yatakayobaki kuuzwa au kuvunjwa kabisa. Ni dhahiri hatua hizo zote zilihitaji ujasiri wa hali ya juu na sote, hapana shaka, tuna deni kubwa kwake.

**Utangulizi:**

4. Mheshimiwa Spika, kikao hiki cha bajeti ambacho ni cha pili tangu kufanyika uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge mwezi Oktoba 1990, na Bunge la pili la awamu ya pili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, pia ni cha kipekee na kihistoria. Ni dhahiri kikao hiki kitakuwa cha mwisho kuendeshwa chini ya Katiba ya nchi ya Chama kimoja. Kama Bunge lako tukufu linavyofahamu, baada ya Tume ya Rais ya kufikiria upya muundo wa siasa wa nchi yetu, ijulikanayo kama Tume ya Nyalali, kumaliza kazi na kukabidhi taarifa yake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, mapema mwaka huu, Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ulikutana mwezi Februari, 1992. Kikao hicho kiliamua kwa kauli moja kubadili mfumo wa siasa wa nchi yetu kutoka ule unaongozwa na Chama kimoja cha siasa kuwa wa Vyama vingi. Baada ya uamuzi huo wa

kijasiri, wenye mtizamo mrefu na mpana, na unaojali zaidi maslahi ya Taifa na watu wake kwa jumla. Bunge lako tukufu nalo likatekeleza wajibu wake wa kihistoria kwa kupitisha, mwezi Mei 1992, pia kwa kauli moja, marekebisho ya Katiba ya nchi yetu ili kutekeleza uamuzi huo wa Chama, ki-sheria. Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu litakubaliana nami kwamba haya ni mageuzi makubwa sana. Hivyo, Chama Cha Mapinduzi, chini ya uongozi thabiti wa Mwenyekiti wake, ambae pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Bunge lako tukufu, chini ya uongozi wako pamoja na Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, ambae ni kiongozi wa shughuli za Serikali katika Bunge, Mheshimiwa John S. Malecela, pamoja na wananchi wa Tanzania, kwa jumla, wanastahili pongezi na shukrani za dhati kabisa, kwa kuyaongoza mageuzi hayo kwa amani na utulivu wa hali ya juu. Hali hiyo inaonyesha wazi jinsi Wa-Tanzania walivyokomaa kisiasa.

5. Mheshimiwa Spika, mbali na mageuzi ya kisiasa, Bunge lako pia limeshuhudia kwa kuidhinisha mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu. Hivyo mwaka 1992/93 utakuwa kipindi muhimu cha kutafakari utekelezaji wa sera zetu za uchumi na za fedha zilizobuniwa chini ya Mipango yetu ya kufufua uchumi. Baadhi ya Sera hizo zimehusisha marekebisho katika sheria mbali mbali zilizopitishwa na Bunge hili katika mwaka 1991/92.

6. Kwa jumla, tangu tumeanza utekelezaji wa mipango yetu ya kufufua uchumi, hatua nyingi muhimu zimechukuliwa ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kuingia katika mfumo wa soko la biashara kutokana na bidhaa mbali mbali, yakiwemo madini, kuingia katika mkondo huo na hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Maeneo yaliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na kuweka mfumo wa uchumi ulio wazi kwa kuruhusu uuzaji na uagizaji bila masharti magumu, kuondoa

ukiritimba katika biashara ya ndani na kuachia bei za mazao ya ndani kuwa katika viwango vinavyowiana na gharama halisi za uzalishaji na usambazaji, kwa kuondoa usimamizi wa bei. Si hiyyo tu, bali Serikali imepanua huduma za ununuzi wa mazao kwa kuwaruhusu wanunuzi katika sekta ya binafsi kununua mazao kutoka kwa wakulima vijijini. Hatua za kuimarisha sekta ya fedha kwa kuondoa vizuizi vya uanzishaji wa benki za binafsi na kufanya marekebisho katika uendeshaji wa benki zilizopo, ikiwa ni pamoja na kuzipa benki hizo mamlaka kamili katika shughuli za utoaji mikopo zimetekelezwa. Kadhalika, hatua za kuleta mabadiliko katika sekta ya mashirika ya umma pia zimechukuliwa ili kuimarisha mchango wake katika maendeleo ya uchumi wetu.

7. Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, katika mwaka 1991/92, Bunge lako tukufu limepitisha sheria kadhaa ambazo zimebadilisha mfumo wa mashirika yetu ya umma ikiwa ni pamoja na mashirika ya fedha. Nitazitaja baadhi ya sheria hizo. **Kwanza,** sheria ya kurekebisha Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 imebadilisha mfumo wa mashirika ya umma na kutoa tafsiri mpya ya Shirika la Umma kuwa ni Shirika ambalo Serikali inamiliki asilimia 51 au zaidi ya hisa na linaweza kujiendesha lenyewe na hivyo kutoa ziada kwa maendeleo ya Taifa na wafanyakazi wake. Kutokana na sheria hiyo imeundwa Tume ya Kurekebisha Sekta ya Mashirika ya Umma, yaani "Parastatal Reform Commission" ambayo pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kuchambua mashirika ya Umma ambayo hisa za Serikali zinatakiwa ziuzwe kwa watu binafsi au kwa kuingia ubia. Aidha, Tume hiyo imepewa jukumu la kufanya uchambuzi na kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kuendesha Taasisi za Serikali kwa ufanisi zaidi.

8. **Pili,** sheria ya kuanzisha 'LART' yaani "Loans and Advances Realization Trust" ambacho ni chombo kinachochambua madeni sugu ambayo mabenki yetu yanadai taasisi za Umma na binafsi na kupendekeza usuluhisho wake kwa lengo la kusafisha vitabu vya hesabu vya mabenki hayo na kuyawezesha kuanza kazi upya katika mazingira ya ushindani. Pamoja na hatua hii, Serikali itafanya kila jitihada ili mabenki haya yapatiwe mitaji ya kutosha ili yaweze kufanya shughuli zao kwa faida. Umuhimu wa hatua hiyo ni katika kuvirudishia vyombo vyetu vya umma mtaji madhubuti wa kuweza kuhimili ushindani utakaotokea baada ya kuruhusu uanzishaji wa vyombo vya fedha vya binafsi kuendesha tena shughuli zao hapa nchini.

9. **Tatu,** sheria ya mabenki ambayo imetubusu uanzishaji wa benki za binafsi na vyombo vingine vya fedha nchini mwetu. Hali hiyo inategemewa kuleta ushindani wa utoaji huduma katika sekta ya fedha na hivyo kuboresha shughuli za ukusanyaji wa amana za wateja na utoaji wa mikopo. **Nne,** sheria ya Fedha za Kigeni imehalalisha umilikaji na ubadilishaji wakati wote wa fedha za kigeni zinazoingizwa nchini katika benki na maduka ya fedha za kigeni. Sheria hiyo imefuta sheria ya kudhibiti fedha za kigeni nchini ambayo ilianza kuwa kero kwa wananchi wengine kulingana na mabadiliko yaliyofanywa katika sera za uchumi. Mabadiliko hayo ambayo yalikwishaanza kutekelezwa yalikuwa ni pamoja na kuruhusu wananchi kuuza mazao na bidhaa nchi za nje na kuingiza bidhaa mbali mbali zinazohitajika hapa nchini. Katika hali hiyo ilikuwa ni rahisi kwa wananchi wafanyabiashara na hata kwa wageni pia kujikuta wamevunja, bila ya kutegemea, baadhi ya vipengele vya sheria ya kudhibiti fedha za kigeni iliyokuwapo. Matokeo yake ilikuwa ni kuzuka kwa soko haramu la kubadilisha fedha za kigeni mitaani ambalo halikuwa na udhibiti wowote. Hali hiyo sasa imebadilika baada ya kutunga sheria ya maduka ya fedha

za kigeni (Bureau du Change) ambayo yameandikishwa rasmi na yanafuata taratibu zilizopitishwa na Bunge hili. Nitaelezea zaidi baadaye mabadiliko hayo ambayo Serikali imeyatekeleza katika sekta za fedha na mashirika ya Umma.

10. Mheshimiwa Spika, hatua hizo zilizochukuliwa zilitokana na juhudi tulizozianza kwa kulegeza masharti ya biashara ambayo yaliwezesha watu binafsi kuingiza bidhaa mbali mbali na kuuza nje mazao yasiyo asilia. Hali hiyo pia imewezesha wahisani kuendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea. Kutokana na hatua hizo, uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo umeendelea kuongezeka, na uuzaji nje pamoja na uagizaji wa bidhaa kutoka nje nao uliongezeka. Katika mwaka 1991/92 tunatarajia kuuza nje mazao yenye thamani ya dola za Kimarekani 422.6 milioni, ikilinganishwa na matarajio ya dola za Kimarekani 393.6 milioni mwaka 1990/91, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.4. Uuzaji halisi wa bidhaa nchi za nje kwa mwaka 1989/90 ulifikia dola za Kimarekani 389.3 milioni.

11. Aidha, uagizaji kutoka nje katika mwaka 1991/92 unatarajiwa kufikia dola za Kimarekani 1,437.4 milioni, ikilinganishwa na matarajio ya uagizaji ya dola za Kimarekani 1,514.8 milioni mwaka 1990/91. Manunuzi halisi kutoka nje mwaka 1989/90 yalifikia dola za Kimarekani 1,360.02 milioni. Ni dhahiri uwiano wa thamani ya bidhaa tunazouza nje na zile tunazoagiza unaonyesha kuwa bado kuna nakisi kubwa, inayozidi dola za Kimarekani 1,000 milioni ikimaanisha kwamba tunaagiza zaidi kuliko tunavyoweza kuuza nchi za nje. Kutokana na hali hiyo, inatubidi kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa tunazosafirisha nje ili ziweze kupata bei nzuri katika soko la dunia, pamoja na kujibana kwa kutoagiza bidhaa na huduma kutoka nje ambazo zinaweza kupatikana hapa hapa nchini.

12. Mategemeo yetu ni kuwa sera ambazo tumeziandaa na kuanza kutekeleza zitazaa matunda zaidi siku za usoni. Mwanzo umekuwa mzuri kwani umeonyesha dalili za uchumi wetu kuibuka kama unavyojionyesha katika ongezeko la thamani ya mazao tunayouza nje. Hata hivyo ni wazi kuwa juhudi zaidi zinahitajika katika kuimarisha huduma hasa za usafirishaji na nyinginezo muhimu kwa sekta zote za uchumi. Hali hiyo inatokana na ukweli kuwa sekta zinategemeana. Juhudi za kufufua sekta moja zinaweza kuathiriwa kama sekta nyingine hazitapewa msukumo unaohitajika wa nyenzo na rasilimali. Hivyo juhudi lazima ziendelezwe hasa katika kudhibiti ongezeko la bei na kuimarisha uchumi wetu katika nyanja zote kwa kuongeza uzalishaji, tija na ufanisi, kupanua mikondo ya biashara na kuimarisha njia za mawasiliano na uchukuzi.

13. Mheshimiwa Spika, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Mipango na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia Mipango, Mheshimiwa Steven Kibona, amekwishaeleza katika Bunge tukufu hili leo asubuhi, hali ya uchumi wa Taifa letu katika kipindi cha mwaka 1991/92. Aidha, ameeleza malengo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 1992/93. Hivyo si nia yangu kurudia yale ambayo ameyaeleza kwa ufasaha, na ningependa kumpongeza tena kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuweka misingi sahihi ya kutafakari bajeti pamoja na mpango wa maendeleo. Kwa hiyo nitazungumzia tathmini ya utekelezaji wa sera mbali mbali za bajeti tulizojiwekea katika mwaka 1991/92 pamoja na bajeti ya Serikali kwa mwaka 1992/93.

Katika kufanya hivyo, itanibidi kugusia jinsi mazingira ya uchumi wetu yalivyochangia utekelezaji wa sera mbali mbali za bajeti ya mwaka 1991/92 na mategemeo kwa mwaka 1992/93.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SERA ZA BAJETI YA MWAKA 1991/92

14. Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika hotuba ya bajeti, Serikali iliazimia kuchukua hatua mbali mbali ili kudhibiti mapato na matumizi yake. Hatua hizo, zilielekezwa katika kurekebisha shughuli za Serikali ili hatimaye mahitaji yake yaweze kutoshelezwa, kwa kiwango cha kuridhisha, na bajeti isiyotegemea mno mikopo kutoka mabenki au kugharamiwa kwa kiwango kikubwa na misaada kutoka nje. Hatua hizo ni pamoja na kufanya marekebisho ya muundo (structure) wa Serikali kwa lengo la kupunguza majukumu yake na kuimarisha ufanisi wa watumishi wake. Aidha, Serikali imedhamiria kurekebisha mfumo wa vyombo vya Umma kwa madhumuni ya kuviwezesha vifanye shughuli zake kwa ufanisi zaidi na bivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kuitegemea Serikali kifedha.

15. Katika mwaka huu wa fedha wa 1991/92 Serikali imeanza kutekeleza baadhi ya hatua hizo. Kwa upande wa Sekta ya jamii hasa elimu ya Sekondari na ya Juu, hatua zimeanza kuchukuliwa za kuwataka wazazi waisaidie Serikali katika kugharamia elimu kwa watoto wao. Aidha, itakumbukwa kuwa mwaka jana Serikali ilianzisha mifuko maalum ya maendeleo kwa ajili ya kusaidia kugharamia huduma mbali mbali za Jamii na za kiuchumi. Mifuko hii ni Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Nyumba, Mfuko wa kupima viwanja na ile ya kusaidia watumishi wa Serikali. Baadhi ya mifuko hii imekwishaanza shughuli zake.

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1991/92, mtaji wa Mfuko wa mikopo ya Magari na vyombo vya nyumbani uliongezwa kutoka Sh. 15 milioni hadi kufikia Sh. 515 milioni. Hata hivyo, pamoja na nyongeza hiyo ya Sh. 500 milioni, bado mfuko huu haukutosheleza

mahitaji. Hivyo Serikali ililazimika kutafuta fedha nyingine za nyongeza. Mbali na hatua hizo, Serikali pia ilichukua hatua za kurekebisha maslahi ya watumishi kadri uwezo ulivyoruhusu. Kwa hiyo viwango vya mishahara na baadhi ya marupurupu viliongezwa.

17. Mheshimiwa Spika, vile vile, maandalizi ya awali yamekamilika ya kuchambua muundo wa Serikali kwa lengo la kuufanyia marekebisho ili kuwa na muundo mdogo lakini wenye ufanisi mkubwa. Kwa upande wa vyombo vya umma, Serikali imeanza uchambuzi wa kina wa Mashirika ya Umma ili kuleta ufanisi zaidi katika vyombo hivi. Serikali imekwishaamua kuwa mashirika ya biashara sasa yaendeshwe kibiashara. Kuhusu Mashirika ya Fedha, hatua kadhaa zimechukuliwa. Itakumbukwa kuwa katika mwaka 1991/92 Serikali ilitoa maelezo kuhusu nia ya kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika sekta hii. Malengo yaliyowekwa yalikuwa ni kuongeza ushindani kati ya vyombo vya fedha ili kuleta huduma nzuri kwa wateja, ikiwa ni mojawapo ya kigezo cha kupima mafanikio ya azma hii. Ili vyombo hivi viweze kufanya shughuli zake za kibiashara kwa ukamilifu, Serikali pia iliazimia kutoingilia shughuli za vyombo hivyo, hasa pale ambapo maagizo ya Serikali yangekwenda kinyume na maadili ya kazi za benki.

18. Mheshimiwa Spika, kwa kukumbushia tu, zipo sababu kadhaa ambazo zilikuwa zimeifanya Serikali kuchukua hatua hizo. Sababu hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:—

(i) Mikopo mingi ya vyombo vya fedha ilikuwa inatolewa nje ya misingi ya kibiashara, na matokeo yake yamekuwa wateja wanaohusika kuendesha shughuli zao bila kuzingatia faida au hasara, na hivyo kushindwa kurejesha mikopo waliyokuwa nayo.

(ii) Mfumo wa vyombo vya fedha uliokuwepo ulishindwa kwa kiasi kikubwa kukusanya rasilimali zilizopo nchini na kuzielekeza katika maeneo ya uzalishaji.

(iii) Vyombo vya fedha vilivyokuwepo vilikuwa na mfumo wa fedha usioridhisha. Mfumo huo ulisababisha ongezeko la ujazi wa fedha katika uchumi wetu na matokeo yake yakawa ni mfumuko wa bei ambao uliathiri kwa kiwango kikubwa hali ya maisha hasa kwa wafanyakazi.

(iv) Kushuka kwa kiwango cha uwajibikaji.

(v) Ukosefu wa ushindani wa kibiashara.

19. Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa inayohusu vyombo vya fedha "The Banking and Financial Institutions Act. 1991" imeanza kutumika rasmi katika mwaka huu wa fedha. Chini ya Sheria hiyo, Benki Kuu (BOT) imepewa majukumu makubwa ya kusimamia utekelezaji wa sheria hii, pamoja na kusimamia vyombo vya fedha nchini ili kuhakikisha kwamba taratibu zinazotakiwa zinafuatwa. Kwa hali hiyo, hatua ya kwanza katika kufanikisha utekelezaji wa sheria hiyo ni kwa Benki Kuu kujiimarisha yenyewe kiutendaji ili iweze kutoa maelekezo na miongozo sahihi kwa vyombo vya fedha vilivyopo na vile ambavyo vitaanzishwa nchini hapo baadae.

20. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya fedha nchini, na ili kufanikisha utekelezaji wa sheria mpya ya vyombo vya fedha ya 1991, Serikali imeanza kushughulikia maeneo mawili makubwa. **Kwanza**, marekebisho ya sera yamefanyika katika vyombo mbalimbali vya fedha kwa kuzingatia misingi ya sheria mpya. Hivyo tayari Benki Kuu imeyapa mabenki uwezo mkubwa zaidi wa kujiwekea viwango vya riba kwa mikopo na amana kwa wateja wao kwa kuzingatia mwongozo wake. Aidha, sera ya viwango vya riba sasa itakuwa inatazamwa mara kwa mara ili viwango

vinavyotolewa vilingane na thamani halisi ya fedha. **Pili,** misingi ya urekebishaji na usimamizi wa shughuli za benki imetayarishwa. Aidha, Benki Kuu imekwishatoa mwongozo na sera ya utoaji leseni kwa ajili ya mabenki na taasisi zingine za fedha. Benki hiyo sasa iko tayari kutoa leseni kwa vyombo ambavyo vina nia ya kuanzisha shughuli zao hapa nchini.

21. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika ya Umma, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali imeteua Tume ya Kurekebisha Sekta ya Mashirika ya Umma ili, kushughulikia vyombo hivi. Baadhi ya majukumu muhimu ya Tume hiyo ni:

(i) Kuchambua mashirika ya umma ambayo hisa za Serikali zinatakiwa ziuzwe au kuruhusu watu binafsi kuingia ubia:

(ii) Kutathmini mashirika ya umma na hivyo thamani ya hisa katika mashirika hayo.

(iii) Kuendesha majadiliano na wale wanaotaka kununua mashirika ya umma au wanaotaka ubia na Serikali.

(iv) Kuishauri Serikali kuhusu taratibu za uuzaji hisa na mashirika ambayo ingefaa serikali iwe na hisa nyingi.

(v) Kufanya uchambuzi na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuendesha Taasisi za Serikali (National Institutions) kwa ufanisi zaidi.

22. Mheshimiwa Spika, kwa jumla pamoja na hatua mbalimbali zilizokwisha chukuliwa hadi sasa, bado kuna kazi kubwa mbele yetu, kwani mahitaji ya Serikali bado ni makubwa mno ikilinganishwa na uwezo wake wa kukidhi mahitaji hayo. Kutokana na hali hiyo, karibu kila eneo la Serikali linapata si zaidi ya nusu ya mahitaji yake halisi. Aidha, kwa upande wa vyombo vya umma, Serikali ilichoweza kukifanya hadi sasa ni kuandaa taratibu za kushughulikia eneo hilo. Hivyo hatua za kuimarisha sekta hii bado hazijachukuliwa kikamilifu.

**Mapitio na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 1991/92:**

23. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya sera mbalimbali zilizoandaliwa na kuanza kutekelezwa katika mwaka 1991/92 naomba sasa nieleze hali ya bajeti ya mwaka 1991/92. Itakumbukwa kuwa katika mwaka 1991/92, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 227,973 milioni ili kugharamia matumizi kwa kiwango hicho. Kati ya mapato hayo, jumla ya Sh. 153,920 milioni zilitazamiwa kutokana na mapato ya kawaida, Sh. 67,953 zikiwa ni misaada na mikopo ya nje, na Sh. 6,100 milioni kutokana na mikopo ya ndani.

24. Hadi kufikia mwisho wa Desemba 1991 jumla ya mapato yote yaliyokusanywa yalikuwa yamefikia Sh. 107,811 milioni. Kati ya fedha hizo, Sh. 76,212 milioni ni mapato ya kawaida, Sh. 26,844 milioni zikiwa mikopo na misaada ya nje, na Sh. 4,755 milioni zikiwa mikopo ya ndani. Kutokana na mwenendo huo pamoja na hatua za marekebisho ya thamani ya fedha yaliyofanyika kuanzia mwezi Aprili 1992, inatarajiwa kuwa mapato yote yatafikia Sh. 262,549 milioni mwisho wa Juni 1992. Kati ya fedha hizo, Sh. 176,614 milioni ni za mapato ya kawaida, Sh. 76,835 milioni ni mikopo na misaada kutoka nje na Sh. 6,100 milioni ni mikopo ya ndani. Kama inavyoonekana jumla ya mapato yote yataongezeka kwa Sh. 34,576 milioni, au asilimia 15.0. Katika ongezeko hili, mapato ya kawaida yatachangia Sh. 22.694 milioni, au ongezeko la asilimia 14.7.

25. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali ilipanga kutumia jumla ya Sh. 227,973 milioni. Kati ya fedha hizo Sh. 189,327 milioni ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 38,646 milioni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kwa upande wa matumizi ya kawaida, matumizi halisi hadi kufikia mwisho wa Desemba 1991 yalifikia Sh. 100,366 milioni. Kutokana na mwenendo huu, inategemewa kuwa matumizi ya kawaida hadi mwisho wa Juni, 1992 yatafikia Sh. 209,560

milioni, ambalo ni ongezeko la Sh. 20,233 milioni, au asilimia 10.7. Aidha kutokana na ongezeko kubwa la karadha kati ya Julai 1991 na Desemba 1991 zaidi ya makisio, Serikali itatakiwa kupunguza limbikizo la mikopo yake kutoka mabenki kwa kiwango cha Sh. 24,259 milioni itakapo mwisho wa Juni 1992, ili kutoathiri malengo ya karadha tuliyojiwekea mwanzo mwa mwaka.

26. Kuhusu matumizi ya maendeleo, matumizi halisi hadi mwisho wa Desemba 1991 yalifikia Sh. 10,104 milioni. Kati ya fedha hizo, Sh. 8,089 milioni ni za ndani na Sh. 2,065 milioni ni za nje. Kufuatana na mwenendo huu, matumizi ya maendeleo hadi mwisho wa Juni 1992 yanatarajiwa kufika Sh. 38,646 milioni. Matumizi ya fedha za ndani yatakuwa Sh. 21,558 milioni wakati fedha za nje zitafikia Sh. 17,088 milioni.

**Majumuisho ya Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 1991/ 92:**

27. Mheshimiwa Spika, kutokana na matarajio ya mapato ya Sh. 262,549 milioni hadi Juni 1992 na matarajio ya matumizi yote (ikiwa ni pamoja na kupunguza deni la mabenki) ya Sh. 272,465 milioni, pengo la Sh. 9,916 milioni linajitokeza. Kati ya pengo hili, Serikali iliidhinisha matumizi ya nyongeza ya Sh. 8,779.3 milioni hapo Mei 1992. Hivyo pengo linalobaki bila ya kufidiwa ni la Sh. 1,136.7 milioni. Kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kupata mapato zaidi ili kufidia pengo hilo, inabidi kila Afisa Mhasibu achukue hatua zitakazomwezesha kumaliza mwaka kwa kiwango cha fedha alizopangiwa.

**Misingi ya Bajeti ya Mwaka 1992/93:**

28. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya hali ya bajeti ya mwaka huu, naomba sasa nieleze misingi ya bajeti kwa mwaka 1992/93. Katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana ilielezwa tatizo sugu linalotokana na mahitaji ya Serikali kuwa makubwa ikilinganishwa na

uwezo wake. Mapato ya ndani ambayo kwa kweli ndiyo uwezo halisi wa Serikali yanakidhi zaidi kidogo ya theluthi moja ya mahitaji halisi ya kuendeshea Serikali. Mikopo na misaada ya kutoka nje imekuwa ikisaidia sana kuiongezea uwezo Serikali kugharamia shughuli zake. Hata hivyo, pamoja na mchango huu wa Wahisani, uwezo uliopo unakidhi si zaidi ya asilimia 50 ya mahitaji halisi.

29. Mbali na tatizo hili, kumekuwa na tatizo jingine la uendeshaji dhaifu wa vyombo mbali mbali vya umma. Jambo hili limelazimisha Serikali kuendelea kubeba mzigo wa madeni makubwa kila mwaka kutokana na hasara za vyombo hivyo. Hali hii imesababisha kasi kubwa ya mahitaji ya fedha ambayo uwezo haumudu. Kwa kuwa mahitaji yote hayo yapo na yanahitaji kugharamiwa, mkakati ambao umekuwa unatumika ni kugawa fedha kidogo kidogo kwa mahitaji yote. Utaratibu huu umefanya huduma zote za Serikali kuwa duni sana. Aidha, ufanisi wa watumishi wa Serikali nao umekuwa hafifu kutokana na vitendea kazi na maslahi duni.

30. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inakabiliwa na tatizo hilo sugu linalotokana na mapato finyu kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayosababishwa na kupanuka kwa haraka kwa shughuli za Serikali. Ni dhahiri tatizo la viwango vidogo vya fedha zinazotolewa kwa ajili ya kuendesha shughuli za Serikali litaendelea kuwapo ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa ili kupunguza mahitaji makubwa ambayo hayalingani kabisa na uwezo wa Serikali wa kukusanya mapato. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, tatizo la Serikali kushughulikia maeneo ambayo yangeweza kutekelezwa na vyombo vingine, limesababisha karibu miradi yote inayotekelezwa kutotengewa fedha za kutosha, hali ambayo inaifanya miradi hiyo ama kutokamilika kwa wakati au hata kutokamilika kabisa.

31. Aidha, kutokana na Serikali kuendelea kuchukua majukumu mengi ambayo haina tena uwezo wa kuyabeba, huduma zitolewazo pamoja na ubora wa huduma hizo umezorota sana. Si hivyo tu, hata miradi inayokamilika hutoa huduma chini ya viwango vilivyokusudiwa. Kadhalika, miradi ambayo imekamilika na kuanza kutoa huduma haifanyiwi matengenezo yanayostahili. Vile vile miradi ya mashirika ya kibiashara inayo madeni makubwa yasiyolipwa kutokana na mitaji midogo pamoja na utendaji usioridhisha. Matokeo ya yote haya yamesababisha uchumi wetu kuendelea kuwa duni kulikoendeleza kasi kubwa ya ongezeko la bei. Ni dhahiri hali hiyo inatulazimisha kuangalia upya maeneo ambayo ni lazima yaendeshwe na Serikali na yale ambayo inabidi iyaachie.

32. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matatizo yote haya misingi ya bajeti ya Serikali ya mwaka 1992/93 imebuniwa kutekeleza mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na Serikali kuchambua upya muundo wake kwa lengo la kuupunguza. Kwa maana hii, Serikali italazimika kubakia na majukumu yake ya kawaida (traditional functions) kwa kiwango ambacho inaweza kuyagharamia kikamilifu. Majukumu hayo ni pamoja na Ulinzi na Usalama wa Raia, Kujenga na kutunza huduma za kiuchumi, Kujenga na kutunza huduma za jamii. Pamoja na kufanya hivyo, wale wanaofaidika na hasa huduma za jamii, itabidi hatimaye wasaidiane na Serikali kwa kuchangia katika uendeshaji wa huduma hizo. Lengo jingine ni kuwa na wafanyakazi Serikalini kiasi lakini wenye tija na ufanisi wa hali ya juu ili waweze kusimamia kikamilifu uandaaji na uratibu wa utekelezaji wa sera mbalimbali za maendeleo ya uchumi na Jamii. Majukumu mengine ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na yale yasiyo ya kodi, kulipa kwa kiwango cha kuridhisha limbikizo la deni la mabenki ambalo Serikali ilikopa miaka ya nyuma, hali ambayo imeongeza sana ujazi wa fedha; kufanya

marekebisho ya mfumo wa mashirika ya Umma ili kuyawezesha kufanya shughuli zao kibiashara na kwa kujitegemea zaidi; na kuwa na mkakati wa uhakika wa kujitoa hatua kwa hatua, katika kutegemea mno misaada kutoka nje.

**Sera Zinazotarajiwa Kutekelezwa Mwaka 1992/93:**

33. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya msingi ya shabaha za bajeti kwa mwaka ujao naomba sasa nieleze sera mbali mbali ambazo Serikali inakusudia kuzitekeleza katika mwaka 1992/93. Kwa Jumla, zipo sera zitakazohusu bajeti ya Serikali, Sekta ya Fedha, Mashirika ya Umma, Sekta za maendeleo ya Jamii na sekta nyinginezo.

**Bajeti ya Serikali:**

34. Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha sema, Bajeti ya Serikali itabidi iainishwe na mahitaji halisi ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya muundo mzima wa Serikali ili ulingane na uwezo. Hivyo ingawa jitihada zitafanyika ili kuongeza mapato ya Serikali kwa kadri itakavyowezekana, itabidi pia mahitaji yachambuliwe upya ili yawiane na uwezo. Kwa maana hii Serikali itazingatia na kuanza kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa ya Tume ya Rais kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali. Taarifa ya Tume hiyo imekwisha chambuliwa kwa kina na Serikali na mengi ya mapendekezo yake yamekubaliwa. Hivyo, kwa niaba ya Serikali, ningependa kuwapongeza Mwenyekiti wa Tume hiyo, Ndugu Edwin Mtei na wana Tume wenzake, kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo hatimaye itaiwezesha Serikali kukusanya mapato zaidi kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo na hivyo kutuongezea pia uwezo wa kujitegemea katika eneo hili.

**Mapato:**

35. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, kama nilivyokwisha sema, Serikali itatekeleza mapendekezo ya Tume ya Kodi ambayo yamekwishafanyiwa maamuzi pamoja na kuchukua hatua nyingine za kuongeza mapato ya Serikali. Kadhalika, Serikali itaimarisha sehemu zinazokusanya maduhuli kwenye Wizara na Mikoa kwa kuweka maafisa wenye ujuzi pamoja na kuwapatia zana za kufanyia kazi. Sambamba na hatua hiyo, tutaimarisha taratibu za kuandaa taarifa sahihi za makusanyo ya mapato hasa kutoka Wizara na Mikoa, ikiwa ni pamoja na kurahisisha na kuimarisha mawasiliano kati yao na Hazina, kuhusiana na ukusanyaji wa mapato hayo.

36. Kuhusu misaada na mikopo kutoka nje, kumekuwa na tatizo la udhibiti hafifu. Serikali imekuwa ikipokea kiwango kikubwa cha misaada hasa vifaa kwa miradi ya maendeleo ambayo wanaoipokea hawaonyeshi thamani yake kikamilifu katika vitabu vya Serikali. Hali hii imesababisha Serikali na Wahisani kuwa na wasiwasi kuhusu udhibiti wa vifaa hivyo. Ili kukabiliana na tatizo hili, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani itaimarisha utaratibu mzima wa kudhibiti misaada hasa vifaa vinavyoletwa na Wahisani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Matumizi:**

37. Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, katika mwaka 1992/93, Serikali itaendeleza jitihada za kurejesha hatua kwa hatua, uwiano mzuri kati ya uwezo na mahitaji. Aidha, katika mwaka 1992/93 Serikali itakamilisha uchambuzi wa majukumu ulioanza mwaka 1991/92. Lengo la uchambuzi huu ni kuiwezesha Serikali kuamua majukumu yapi iendelee kuwa nayo na yapi iyaachie vyombo vingine ambavyo vitaweza kuyashughulikia kwa ufanisi zaidi. kadhalika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Serikali imekuwa na

miradi mingi mno kiasi kuwa ni vigumu kuipatia fedha zote zinazohitajika. Hali hii imesababisha matatizo makubwa mawili. **Kwanza** kama nilivyoeleza hapo awali, kumekuwa na miradi mingi ya viporo ambayo imekuwa haikamiliki kwa miaka mingi sasa kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha. **Pili** kutokana na wingi wa miradi imekuwa vigumu kusimamia kikamilifu utekelezaji wake. Ili kurekebisha hali hii Serikali itafanya uchambuzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo ambayo inaigharamia ili kuipunguza na hivyo kuwa na hakika zaidi wa utekelezaji wake kuliko ilivyo sasa.

38. Mheshimiwa Spika, sambamba na uchambuzi huu, Serikali pia inaangalia upya suala la ajira yake. Eneo hili limekuwa na matatizo mengi. Kumekuwa hakuna udhibiti wa kutosha katika uajiri wa watumishi. vyombo vinavyoajiri ni vingi mno na imekuwa vigumu kuviratibu kwa pamoja. Matokeo yake, watumishi zaidi, hata katika zile kada ambazo imekubalika wasiajiriwe tena, bado wanaendelea kuajiriwa. Kadhalika, kutokana na uwezo wa Serikali kifedha kupungua mwaka hadi mwaka imekuwa vigumu kuwalipa watumishi maslahi ya kuridhisha. Tatizo la maslahi duni ya watumishi linajidhihirisha katika kiwango kidogo cha ufanisi wa watumishi hao. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hili, Serikali kwa mwaka 1992/93 itaweka utaratibu madhubuti wa kudhibiti ajira yake. Aidha, kuanzia mwaka 1992/93 Serikali pia itaanza kwa kuwasaidia baadhi ya watumishi wa Serikali ambao wameonekana dhahiri kuwa wamezidi mahitaji, kujitafutia shughuli nyingine za kufanya *(redeployment)*.

39. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Serikali inalazimika kuchukua hatua hiyo ya kuwasaidia kujitafutia shughuli nyingine za kufanya baadhi ya watumishi wake kutokana na sababu kubwa mbili. **Kwanza,** kutokana na uchunguzi wa kina uliofanyika na Idara Kuu ya Utumishi Serikalini, imeonekeana kwamba ingawa katika baadhi ya maeneo, kwa mfano walimu,

kuna upungufu wa zaidi ya wafanyakazi 16,000 katika maeneo mengi yaliyobaki kuna watumishi zaidi ya 80,000 katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambao wanazidi mahitaji ya kazi zilizopo za kufanya. Ni wazi basi Serikali haiwezi tena kuendelea kukwepa kuchukua hatua zinazostahili ili kurekebisha hali hiyo. **Pili,** kutokana na mageuzi makubwa ya kiuchumi yanayoendelea kufanyika, majukumu ya Serikali yamekuwa yakipungua na yataendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Hivyo ukubwa wa Serikali, kwa maana ya Idara zake na watumishi, hauwezi kuendelea kama ulivyokuwa wakati tulipokuwa, kwa mfano, na mashirika ya umma ya kusimamia, zaidi ya 300, hata kama mashirika hayo sasa yatapungua sana kutokana na mengi yake kuingizwa katika ubia, kuuzwa au hata kufungwa kabisa.

**Deni la Taifa:**

40. Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo linapunguza sana uwezo wa Serikali ni deni la Taifa. Kiwango cha deni la Taifa kimeongezeka sana tukijumlisha deni la ndani na la nje. Kwa upande wa deni la ndani, hili linaongezeka kutokana na Serikali kuendelea kukopa kutoka vyombo vya fedha ili kukidhi matumizi. Kama nilivyokwisha sema hapo awali, njia pekee ya kupunguza deni la ndani ni kufanya marekebisho ya muundo wa Serikali ili gharama za uendeshaji wake ziweze kufidiwa na mapato. Kuhusu deni la nje, hili linaongezeka kwa kasi kubwa, kutokana na kurekebisha thamani ya fedha yetu pamoja na ongezeko la madeni mapya. Ingawa baadhi ya wadai wamesamehe madeni yao na wengine kuahirisha malipo bado kiwango cha deni ni kikubwa mno.

41. Ni muhimu nieleze kuwa uahirishaji wa madeni ya nje hautoi nafuu kwa bajeti ya Serikali, bali ni kwa urari wa malipo ya nje *(Balance of Payments)*. Mikataba ya kuahirisha madeni inataka Serikali iendelee kulipa

madeni yote Benki Kuu kwa fedha za Tanzania, kama utaratibu wa malipo unavyohitaji. Ni wazi hali hii haitoi unafuu kwa bajeti ya Serikali. Jitihada za kuwataka wahisani wakubali kuwa uahirishaji wa madeni uyahusu pia malipo ya madeni kwa fedha za Tanzania zinaendelea ingawa hazijafanikiwa. Uamuzi sahihi wa tatizo hili la madeni ni kuacha kuendelea kukopa madeni yenye muda mfupi wa kupevuka, na kupunguza ukopaji kwa jumla.

42. Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo hilo la madeni ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru, kwa niaba ya Serikali, Wahisani mbalimbali ambao wamekuwa wakisaidia harakati zetu za maendeleo kwa miaka mingi sasa. Ni dhahiri misaada yao imechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio tuliyonayo. Aidha, inabidi nikiri kuwa misaada hiyo imekuwa kichocheo kwetu katika juhudi zetu za kuendeleza uchumi. Wahisani hao ni Benki ya Dunia, Swedeni, Denmark, Norway, Ujerumani, Uholanzi, Finland, EEC, Japan na Uingereza. Wengine ni Italia, France, China, Korea, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Canada, Marekani, Belgium, UNDP na mashirika mengine ya Umoja wa mataifa, IMF, OPEC, IFAD, EIB, Saudi Fund, Kuwait Fund, BADEA, Switzerland, Iran, Hispania na Ireland.

**Sekta ya Fedha:**

43. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zilizokwisha fanyika kuboresha sekta hii, Serikali inatarajia kuchukuwa hatua zaidi ili kuimarisha. Baadhi ya hatua inazotegemea kuchukuwa ni kuangalia upya miundo ya benki na taasisi nyingine za fedha ili kuziweka tayari kwa ushindani wa kibiashara. Madeni sugu ya mabenki yatachambuliwa kwa lengo la kuyaondolea mzigo huo mabenki yetu yanayohusika. Aidha, Serikali itahakikisha inatoa kiwango cha mtaji wa kuridhisha ili kuweka msingi *(capital base)* bora wa kuendesha biashara. Katika kufanikisha azma hiyo ya kuyapatia

mabenki yetu mtaji wa kutosha itabidi mali ya vyombo hivyo ichambuliwe na sehemu yake kuuzwa ili kuchangia katika kupata mtaji wa kutosha kwa chombo kinachohusika.

44. Kuhusu uanzishaji wa vyombo vya fedha vya binafsi, Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje ili kuwekeza katika sekta hii. Taarifa za awali zinaonyesha kuwa tayari wamekwishajitokeza wawekezaji kadhaa wa ndani na nje ya nchi wanaotaka kuanzisha mabenki na vyombo vingine vya fedha hapa nchini. Benki Kuu inafanya uchambuzi wa kina wa maombi ya wawekezaji hao kwa lengo la kuwakubalia endapo watakuwa wametimiza masharti yaliyowekwa.

**Mashirika ya Umma:**

45. Mheshimiwa Spika, hapo awali nilieleza kwamba katika mwaka wa 1991/92 Serikali tayari ilikwisha chukuwa baadhi ya hatua muhimu za kurekebisha sekta hii. Hata hivyo, bado tunahitajika kuchukuwa hatua zaidi ili kuleta ufanisi. kwa hiyo katika mwaka 1992/93 masuala muhimu yatakayoshughulikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina wa thamani ya mali ya baadhi ya Mashirika kwa lengo la kuingia ubia na wawekezaji binafsi watakaotaka kuwekeza katika mashirika hayo. Kazi hiyo itafanywa na Tume ya Mashirika ya Umma ambayo tayari imeundwa. Aidha, Serikali kwa kupitia chombo chake cha *"Loans and Advances Realization Trust (LART)"* itafuatilia kikamilifu madeni ya mashirika mbalimbali na kuandaa mkakati wa kuyalipa. Hii ni pamoja na kufilisi au kufunga baadhi ya vyombo hivyo endapo itaonekana hakuna njia ya kuviokoa.

**Sekta Binafsi:**

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali za kuimarisha sekta hii ili hatimaye ichukuwe sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi hapa

nchini. Hii ni pamoja na kutoa sera mpya ya uwekezaji kurekebisha mfumo wa vyombo vya fedha, pamoja na kuruhusu sekta binafsi kuanzisha vyombo vyake vya fedha. Aidha, sheria ya makampuni inafanyiwa marekebisho ili kukidhi mwelekeo huo mpya. Ili kuvifanya vyombo vya Umma vimilikiwe na umma wenyewe moja kwa moja, Serikali katika mwaka 1992/93 itashughulikia pia uanzishaji wa soko la mitaji (capital/ stock market). Kuwepo kwa soko hilo kutawawezesha wananchi wengi kujinunulia hisa katika mashirika mbalimbali na hivyo kuweza kuyamiliki wao wenyewe moja kwa moja badala ya kuyamiliki kupitia Serikali. Kadhalika, soko la mitaji litasaidia mashirika mbalimbali kupata rasilimali ya kutosha hasa katika kipindi hiki ambacho uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji haya umekuwa finyu sana. Pamoja na umuhimu wa kuwa na soko hili, itabidi kufanya maandalizi kabambe ya kuelimisha umma maana na faida ya soko hili kwao, kazi ambayo itapewa kipaumbele katika mwaka 1992/93.

**Maslahi ya Watumishi wa Serikali:**

47. Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa sasa Serikali imekuwa ikiongeza viwango vya mishahara na marupurupu mbali mbali kwa watumishi wake. Lengo la hatua hiyo ni kuwasaidia watumishi hao, angalau kwa kiwango fulani, kuweza kumudu hali ya maisha. Ni kweli kabisa kwamba viwango hivyo vya mishahara bado havijawezakuwiana hata kidogo na hali halisi ya maisha. Ningependa kusisitiza hata hivyo kwamba viwango hivyo vya mishahara vimekuwa vikitolewa kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Serikali kifedha, pamoja na kudhihirisha dhamira ya Serikali ya kuwapatia nafuu ya maisha watumishi wake kila hali inaporuhusu kufanya hivyo. Kutokana na idadi kubwa ya watumishi ambayo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, mahitaji ya mishahara na marupurupu nayo yamekuwa

yakiongezeka sana, hali ambayo imefanya uwiano wa mapato na matumizi ya Serikali ambao tayari umekuwa hauridhishi kwa miaka mingi kuzidi kuwangumu zaidi.

48. Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza, katika jitihada za kukabiliana na tatizo la hali ngumu ya maisha linalowakabili watumishi wake hususan wale wa kipato cha chini, katika mwaka 1992/93, Serikali inakusudia kufanya marekebisho ya viwango vya sasa vya mishahara ya watumishi wake, kulingana na uwezo wake kifedha. Hivyo kutokana na azma hiyo, kuanzia tarehe 1/7/92, kima cha chini cha mshahara cha Sh. 3,500/- kitaongezwa hadi kufikia Sh. 5,000/- kwa mwezi, ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 42.8. Kwa viwango vingine vya mishahara ongezeko litakuwa kidogo ingawa halitakuwa chini ya asilimia 15. Kwa jumla viwango vingine vya mishahara vitarekebishwa na Idara Kuu ya Utumishi hapo baadaye ili kuleta uwiano unaotakiwa.

**Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 1992/93:**

49. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya msingi ya bajeti na sera mbali mbali ambazo Serikali inanuia kutekeleza mwakani, naomba sasa nielezee mfumo wa bajeti kwa mwaka 1992/93. Kwa kuzingatia hali yetu ya uchumi ilivyo, Serikali mwaka 1992/93 imepanga kutumia jumla ya Sh. 353,605 milioni. Katika fedha hizo, Sh. 251,543 milioni ni kwa matumizi ya kawaida na Sh. 102,062 milioni ni kwa matumizi ya maendeleo. Mchanganuo kamili wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo:—

**A. Matumizi ya Kawaida:**

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Mfuko Mkuu (CFS) ................ | Sh. 80,022.5 milioni |
| (ii) | Wizara/Idara ........................ | Sh. 90,397.9 milioni |
| (iii) | Mikoa ................................. | Sh. 10,520.4 milioni |
| (iv) | Halmashauri ......................... | Sh. 23,452.2 milioni |
| | — Wilaya ....... | Sh. (19,566.7) milioni |
| | — Miji ............ | Sh. (3,886.5) milioni |
| (v) | Matumizi Maalum ................ | Sh. 47,149.0 milioni |
| | Jumla ya Matumizi ya Kawaida ... | Sh. 251,543.0 milioni |

## B. Matumizi ya Maendeleo:

| | Jumla Sh. | Fedha za Ndani Sh. | Fedha za Nje Sh. |
|---|---|---|---|
| Matumizi ya Maendeleo . | 102,062.0m. | 30,000m. | 72,062m. |
| (i) Wizara ............... | 89,143.0m. | 24,756m. | 64,387m. |
| (ii) Mikoa ............... | 10,470.0m. | 2,795m. | 7,675m. |
| (iii) Halmashauri ...... | 2,449.0 | 2,449m. | — |

Jumla ya Matumizi yote Sh. 353,605.0 milioni.

50. Mheshimiwa Spika, matumizi haya ya Sh. 353,605 milioni yanaonyesha ongezeko la asilimia 55 ikilinganishwa na makisio ya mwaka 1991/92 ya Sh. 227,973 milioni au asilimia 29 ikilinganishwa na matarajio ya matumizi ya Sh. 272,465 kwa mwaka huu. Sababu kubwa za ongezeko hilo ni kuongezeka kwa deni la Taifa, marekebisho ya utaratibu wa kudhibiti misaada na mikopo kutoka nje hasa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na ongezeko katika matumizi maalum. Kama ilivyoelezwa hapo awali, deni la taifa limepangwa kugharimu Sh. 80,022.5 milioni sawa na ongezeko la asilimia 32 ikilinganishwa na matarajio ya Sh. 60,386.2 milioni kwa mwaka 1991/92.

51. Matumizi ya maendeleo, nayo yanaonyesha ongezeko la asilimia 164 ikilinganishwa na matarajio ya Sh. 38,646 milioni kwa mwaka 1991/92. Hii ni kutokana hasa na uamuzi wa Serikali, kwa kushirikiana na Wahisani, kuweka kiwango sahihi cha mikopo na misaada kwa ajili ya matumizi ya maendeleo katika makisio. Kwa miaka ya nyuma tulikuwa tunaweka kiasi kidogo mwanzoni mwa mwaka na baadaye kuomba Bunge kuidhinisha nyongeza ya matumizi wakati tunapopata misaada zaidi kuliko tulivyokisia. Hali hii kama nilivyoeleza hapo awali imeleta matatizo katika udhibiti wa bajeti hasa pale ambapo baadhi ya sekta zinazopata misaada hii haziingizi kikamilifu katika vitabu vya Serikali.

52. Kuhusu matumizi maalum, haya yameongezeka kutokana na mahitaji ya kugharamia nyongeza za mishahara, mbolea na akiba ya chakula ya Taifa (SGR), marekebisho ya vyombo vya fedha, ufufuaji wa baadhi ya mashirika na malipo ya madeni ya vyombo vya Serikali; Wizara na Mikoa pamoja na mashirika ya Umma. Mahitaji ya vyombo hivi kwa pamoja yanachukua zaidi ya Sh. 37,561 milioni kati ya Sh. 47,149 milioni za matumizi maalum sawa na asilimia 80. Sehemu inayobaki ni kwa ajili ya mfuko wa dharura na mahitaji mengine kama vile maafa, njaa, mafuriko, mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza na mengineyo.

53. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, inategemewa kuwa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi bila ya kurekebisha sera na viwango vya kodi mbali mbali yatafikia jumla ya Sh. 199,607 milioni. Kati ya fedha hizi, Sh. 184,606 milioni zinatokana na mapato ya kodi na Sh. 15,001 milioni ni kutokana na mapato yasiyo ya kodi. Kuhusu misaada na mikopo ya nje, hii imepangwa kuchangia jumla ya Sh. 140,998 milioni. Hivyo, mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na mikopo na misaada kutoka nje yatafikia jumla ya Sh. 340,605 milioni. Mapato haya yakilinganishwa na matumizi ya Sh. 353,605 milioni, pengo la Sh. 13,000 milioni linajitokeza ambalo inabidi lifidiwe na vianzio vingine vya mapato.

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1992/93 Serikali inategemea kupata mikopo isiyo ya mabenki ya jumla ya Sh. 7,000 milioni. Aidha, kutokana na ongezeko kubwa la ujazi wa fedha mwaka huu wa 1991/92 kuliko ilivyopangwa, tunalazimika tena kuchukua hatua ya kupunguza ongezeko la Karadha kwenye uchumi ili kudhibiti mfumuko wa bei. Ili kufanikisha azma hii, Serikali inalazimika kupunguza limbikizo la deni lake kwa mabenki kwa kiasi cha Sh. 10,000 milioni. Hivyo, kwa kuzingatia mapato ya mikopo isiyo

ya mabenki ya Sh. 7,000 milioni na mahitaji ya marejesho ya mikopo ya mabenki ya Sh. 10,000 milioni pengo la bajeti ambalo itabidi lifidiwe na njia nyingine za mapato linakuwa Sh. 16,000 milioni.

**Hatua za Mapato Mapya:**

55. Mheshimiwa Spika, kabla sijatangaza hatua za kuipatia Serikali mapato mapya, ili kuweza kuziba pengo la Sh. 16 bilioni, napenda kwanza nilieleze Bunge lako Tukufu, na kwa kupitia Bunge hili kuwatangazia wananchi na wengine, kuhusu sera na mifumo ya kodi ambayo Serikali inakusudia kuifuata kuanzia mwaka ujao wa 1992/93 na kuendelea.

**Sera Mpya za Kodi:**

56. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, katika jitihada za kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii, tumekuwa tunatunga sheria kadhaa za kodi ili kufanikisha madhumuni na malengo ya sera mbali mbali. Baadhi ya malengo ya sera na kodi hizo ni pamoja na:—

(i) Kuleta usawa au uwiano mzuri wa mapato miongoni mwa Watanzania;

(ii) Kuvisaidia viwanda vyetu dhidi ya mashindano ya bidhaa zinazotoka nje.

(iii) Kuitafutia Serikali mapato zaidi, mwaka hadi mwaka, ili kukidhi mahitaji ambayo yamekuwa yanaongezeka kila mara.

57. Mheshimiwa Spika, kutokana na sera hizi pamoja na ufinyu wa maeneo ya kutoza kodi (narrow tax base) tumejikuta kila mara tunaongeza viwango vya kodi. Matokeo ya hatua hizi ni kwamba ingawa kwa muda fulani ziliweza kufanikisha malengo, lakini vile vile baada ya miaka mingi kumetokea pia athari mbali mbali. Kodi hizo, kwa sehemu fulani, zimepunguza mapato halisi ya wafanyakazi na wananchi kwa jumla. Kadhalika, kwa

kiwango fulani pia, kodi hizi zimeathiri uzalishaji katika baadhi ya viwanda vyetu kwa kuongeza gharama na hivyo kufanya bei za bidhaa zetu kuwa kubwa kuliko zile za bidhaa za kutoka nje. Aidha, wingi wa kodi zetu na ukubwa wa viwango vyake umeshawishi baadhi ya wafanyabiashara kutumia kila njia kukwepa ulipaji kodi, na wengine wamekuwa wanaomba misamaha ya kodi. Hali hiyo imesababisha kuwepo udhaifu na ufanisi mdogo wa utendaji wa Idara zetu za kodi katika kukusanya mapato, na suala la rushwa limeanza kujitokeza katika Idara hizo.

58. Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, ili kufufua na kukuza uchumi wetu lazima hali ya mifumo ya kodi za sasa, irekebishwe. Mfumo wa kodi unaotakiwa wakati huu ni ule unaomhamasisha mlipa kodi kulipa badala ya kumfanya kutafuta njia za kukwepa kodi, au hata kumfanya atafute na kuomba msamaha ili asilipe kodi. Tunahitaji pia mfumo wa kodi usioathiri uzalishaji katika viwanda na katika sekta nyingine pia. Wakati huo huo tunahitaji kuhakikisha mfumo huo unaleta ufanisi na hivyo kutoa huduma au kuzalisha bidhaa bora zenye bei nafuu siyo tu kwa mlaji wa ndani bali pia ziweze kuuzika katika masoko ya nje. Tunahitaji pia mfumo wa kodi wenye vivutio vya kuhamasisha watu kuwekeza rasilimali zao hapa nchini..

59. Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo na misingi hiyo niliyoitaja, Serikali imelitafakari kwa kirefu suala hili, kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mapato na Matumizi ya Serikali, pamoja na maamuzi mengine ya Serikali, ninapenda kulitangazia Bunge lako tukufu kuwa Serikali imefanya maamuzi muhimu katika maeneo ya kupunguza viwango vya kodi, kuondoa na kurekebisha misamaha ya kodi pamoja na kufuta baadhi ya kodi.

**Kupunguza viwango vya Kodi:**

60. **Kwanza** ni kuwa Serikali imeamua kupunguza kwa asilimia kumi (ten percentum) ukubwa wa viwango vya kodi zifuatazo: ushuru wa forodha; kodi ya mauzo; na kodi ya mapato. Kuhusu ushuru wa forodha, viwango vya sasa ni '0', 20%, 30%, 40%, na 60%. Kuanzia kesho tarehe 19 Juni, 1992 viwango hivyo vitateremshwa na vitakuwa ni '0', 10%, 20%, na 40%. Kwa upande wa kodi ya mauzo viwango vipya vitakuwa ni '0', 10%, 20%, na 30% ikiwa ni kiwango cha juu kabisa, badala ya viwango vya sasa. Viwango vya kodi ya mapato vitashushwa pia. Kwa mlipa kodi binafsi, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi, viwango vyake (marginal rates) sasa vitakuwa kuanzia 5% mpaka 30% badala ya vile vilivyopo hivi sasa vya 7.5% mpaka 40%. Aidha, **malipo ya pensheni kwa wastaafu pamoja na yale ya NPF, PPF na GEPF hayatatozwa kodi yoyote.**

61. Kodi ya makampuni ya humu nchini nayo inateremshwa kutoka 45% kuwa 35% ambapo yale ya kigeni, kiwango chake kitashuka kutoka 50% kuwa 40%. Vile vile makampuni ya kigeni yenye ubia na yale ya humu nchini (Joint Ventures), viwango vyake vitakuwa ni 35% sawa na kiwango kitakacholipiwa kodi na makampuni ya humu nchini. Mabadiliko hayo ya kodi ya mapato yataanza kutumika tarehe 1 Julai, 1992, kwa viwango vya kodi vinavyotozwa kwa watu binafsi; na kwa viwango vya makampuni, tarehe ya kuanza itakuwa tarehe 1 Januari 1993. Madhumuni ya Serikali katika kupunguza kodi hizo, ni kumpa nafuu mlaji, na kupunguza gharama za uzalishaji. Aidha kupunguza viwango vya kodi ya mapato kutawawezesha watu na makampuni kupata zaidi mapato na faida ambazo inatumainiwa watatumia kuwekeza na hivyo kukuza uchumi kwa jumla. Vile vile ni matarajio ya Serikali kuwa

kwa vile kodi zimeteremshwa walipakodi watahamasika kulipa kodi zao bila kusita au kuchelewa, na kwa njia hiyo kutunisha mapato ya Serikali.

62. Pili, Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yatafanywa katika viwango vya ushuru wa "excise". Hivi sasa mbali na "Specific rates" zilizopo kuna viwango vingi vingine ambavyo vinaanzia 10%, 25%, 30%, 50%, 60%, 75%, 80%, na 85%. Viwango hivyo vyote vinafutwa na tunabakiza kiwango cha 20%, ambacho kitatumika badala ya hivyo vya sasa. Bidhaa zilizokuwa zinatozwa kiwango cha chini ya 20%, hazitatozwa tena kodi hiyo. Kuhusu vile viwango vya "Specific" marekebisho yamefanywa ili kuvipunguza kama Waheshimiwa Wabunge watakavyoona na kusoma katika Muswada wa Fedha 1992. Kodi hii ya (excise) imeondolewa kabisa kwa bidhaa zinazozalishwa humu nchini za sukari, sabuni, nguo, viberiti, magodoro, na saruji.

63. Uamuzi wa tatu, Mheshimiwa Spika, ambao Serikali imeufanya unahusu kuondolewa kabisa kwa kodi kwa malighafi zote (raw materials) zinazotumiwa katika uzalishaji wa bidhaa katika viwanda humu nchini. Kuanzia kesho tarehe 19 Juni, 1992 hakuna malighafi yoyote ile, iwe kutoka nje au itakayo nunuliwa humu nchini kutoka viwandani, itakayotozwa ushuru wa forodha au kodi ya mauzo. Lengo la hatua hii ni kuvirahisishia viwanda vyetu kupata malighafi na kuvipunguzia gharama za uzalishaji na hivyo kuviongezea uwezo wa kushindana katika soko la ndani pamoja na masoko ya nje.

64. Mheshimiwa Spika, uamuzi wa nne, ni kuwa kuanzia kesho, Serikali imeondoa kodi zote za ushuru wa forodha na kodi ya mauzo kwa magari ya mizigo na mabasi yenye uwezo wa kubeba mzigo wa tani tatu au zaidi au abiria wasiopungua ishirini na tano. Sharti pekee

la msamaha huu ni kuwa mabasi au malori hayo lazima yawe mapya. Magari ya aina hiyo ambayo ni ya zamani yatalipiwa viwango vipya vya asilimia kumi (10%) vya ushuru wa forodha na kodi ya mauzo. Kwa upande wa vipuri ambavyo ni maalum kwa magari hayo, viwango vimeteremshwa na vitakuwa viwango vya asilimia 10% pia.

**Kuondoa na Kurekebisha Misamaha ya Kodi:**

65. Mheshimiwa Spika, uamuzi wa **tano** uliofanywa na Serikali unahusu misamaha ya kodi. Baada ya kuteremsha viwango hivyo vya kodi mbali mbali kama nilivyoeleza, na vile vile baada ya kuondoa kodi kwa malighafi, mabasi, malori na kuteremsha kodi kwa vipuri, misamaha mingi ya kodi sasa inabidi ifutwe. Kwa hiyo Serikali imeamua kuanzia kesho tarehe 19 Juni, 1992 kufuta misamaha yote ya kodi iliyokuwa inatolewa kwa Serikali yenyewe, Serikali za Mitaa, Vyama vya Siasa na Jumuiya zake. Aidha Mashirika na Makampuni ya biashara yote nayo sasa yatatakiwa kulipa kodi. Hali kadhalika mashirika ya dini nayo yatalipa kodi isipokuwa kwa vifaa ambavyo vinatumika moja kwa moja katika sala. Kwa upande wa Mashirika ya kujitolea (NGOs and charitable organizations) nayo yatalipa kodi isipokuwa kwa zawadi (donations) ambazo wataletewa au kupewa ili mradi bidhaa au vifaa vitakavyohusika vitatolewa au kugawiwa **bure** kwa maskini (the needy and the poor). Kwa baadhi ya maeneo misamaha hiyo itaangaliwa upya ili kuipunguza au kuziba mianya iliyopo. Mfano wa hili ni misamaha inayotolewa kwa walemavu au watu wanaopatwa na maafa (disasters). Hatua hii, ya kuondoa na kuirekebisha baadhi ya misamaha ya kodi, itapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yaliyopo hivi sasa kuhusiana na misamaha hiyo.

**Kufuta kodi:**

66. Mheshimiwa Spika, uamuzi wa **sita** ambao umefanyika ni kufuta kodi nyingine pia ambazo zimepitwa na wakati. Kodi hizo ni mbili: ya kwanza ni ile ya "foreign travel levy" ambayo hutozwa kwa kiwango cha 20% kutegemea bei ya tiketi za ndege. Lengo la kuweka kodi hii mnamo mwaka 1979/80 ilikuwa kujaribu kupunguza watu wasisafiri sana nje, na kwa hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Kufuatana na mabadiliko ya sheria ya Fedha za Kigeni, iliyopitishwa na Bunge hili mwanzoni mwa mwaka huu, hakuna tena haja ya kuwabana watu wanaotaka kwenda nje. Hivi sasa watu hao wanabanwa na malipo ghali wanayolipa kutokana na kukata tiketi kupitia maduka ya 'Bureaux de Change'. Hivyo sheria hii inapendekezwa ifutwe kwa vile madhumuni na haja ya kuwa na kodi hiyo haipo tena.

67. Kodi ya pili inayopendekezwa kufutwa ni ile inayotozwa kwa mtaji (Tax on Share Capital). Mheshimiwa Spika, Bunge lako litakumbuka kwamba kodi hii hutozwa kwa wale wote wanaoanzisha na kuandikisha makampuni kufuatana na mtaji. Kiwango chake ni 1% na hulipwa pia wakati mtaji wa kampuni unapoongezwa. Wengi kwa kutaka kukwepa kodi hii huwa wanataja na kuandikisha mtaji mdogo hata kama shughuli zake zinahitaji mtaji mkubwa zaidi. Aidha wale ambao wanataka kuongeza mtaji huacha kujiandikisha kwa kuhofia kodi hiyo na hasa mtaji unapokuwa ni mkubwa sana. Hivyo mbali na wengi kukwepa, wengine na hasa wawekezaji katika miradi mikubwa wamekuwa wanalalamika. Vile vile kodi hii inapingana na sheria ya uwekezaji rasilimali. Hivyo inapendekezwa kodi hii pia ifutwe.

## Mapato Mapya:

68. Mheshimiwa Spika, baada ya kulitangazia Bunge lako tukufu juu ya sera mbali mbali za kurekebisha mifumo ya kodi na kuteremsha viwango au kuondoa kodi kwa baadhi ya bidhaa, hususan malighafi kwa viwanda na kodi za magari (mabasi na malori) pamoja na kufuta baadhi ya sheria za kodi, ningependa sasa kuelezea juu ya hatua mpya zinazokusudiwa kuchukuliwa na Serikali na ambazo zinapendekezwa kwa Bunge hili ili kupata mapato mapya ya zaidi ya Sh. 16,000 milioni ili kuziba pengo lililojitokeza katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka 1992/93.

69. Mheshimiwa Spika, hatua hizo mpya zinahusu maeneo makubwa matatu: Eneo la kwanza linahusu mapato yatokanayo na kodi, eneo la pili ni lile la mapato yasiyo ya kodi; na eneo la tatu ni la kuimarisha mbinu za kukusanya mapato.

## Mapato yatokanayo na Kodi:

70. Mheshimiwa Spika, katika eneo la kodi, Serikali inapendekeza: Kwanza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Huduma za Kiwanja cha Ndege (The Airport Service Charges Act, 1962). Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuwa kile kiwango cha kodi hii cha dola za Kimarekani ishirini (USD 20) kinachotozwa kwa wasafiri wageni (non-residents) kwenda nje, sasa kitozwe pia kwa wasafiri wa hapa nchini (residents) wanaokwenda nje kwa vile hakuna mtu anasafiri nje ya nchi bila ya fedha za kigeni. Hatua hii haitawahusu abiria walio 'transit' kwa muda usiozidi saa ishirini na nne (24). Mheshimiwa Spika, hili litaipatia Serikali Sh. 72 milioni za ziada. Badiliko hili linaanza kutumika kuanzia kesho tarehe 19 Juni, 1992.

71. Sheria ya Ushuru wa Kupanda Meli (The Port Service Charges Act, 1974). Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuwa wasafiri wa meli katika bahari na maziwa kwa safari za humu humu Tanzania, kati ya mji na mji mwingine, sasa nao wawe wanatozwa Sh. 300/- kwa kila abiria anapoondoka na meli. Wageni (non-residents) watalipa dola za Marekani tano (USD 5). Aidha kiwango cha sasa kinachotozwa kwa abiria wanaosafiri kwa meli kwenda nje ya nchi (foreign destinations) sasa kiongezwe kutoka Sh. 20/- kuwa Sh. 300/-. Mheshimiwa Spika, hatua hii haitawahusu abiria katika vivuko (ferries) katika mito au katika maziwa. Hatua hii inatarajiwa itaiingizia Serikali mapato ya Sh. 5 milioni. Mheshimiwa Spika, hatua hii imechukuliwa sambamba na hatua kama hii ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua. Badiliko hili linaanza kesho tarehe 19 Juni, 1992.

72. Hatua ya tatu ni kuongeza kiwango cha "Road Toll" kinachotozwa kwa mafuta ya dizeli na petroli. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kiwango cha sasa cha Sh. 7/- kwa lita. kiongezwe kuwa Sh. 10/-. Jumla ya mapato mapya yanayotarajiwa kwa hatua hii ni Sh. 1,353 milioni. Mheshimiwa Spika, fedha hizi zitaingizwa katika Mfuko wa Barabara (Road Fund) kwa ajili ya ujenzi na utengenezaji wa barabara zetu chini ya mradi wa IRP.

73. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ya kodi inahusu sheria ya Ushuru wa Forodha (The Customs Tarrif Act, 1976). Inapendekezwa kuanza kutoza ushuru wa asilimia ishirini (20%) mafuta yanayotoka nje ya kulainishia mashine na mitambo (lubricants). Lengo la hatua hii, mbali ya kuipatia Serikali mapato, ni kutaka kulinda kiwanda chetu cha mafuta hayo kilichopo Kurasini. Jumla ya Sh. 252 milioini zinakadiriwa zitapatikana kwa hatua hii.

74. Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ya kodi ambayo inapendekezwa kufanyiwa mabadiliko kwa madhumuni ya kuiongezea Serikali mapato ni ile ya Kodi ya mapato, (The Income Tax Act, 1973). Kuna mabadiliko matatu:

(i) Inapendekezwa kuwa sheria ibadilishwe ili kuvitaka vyombo vya fedha, hususan mabenki, yaanze kulipa kodi kwa njia ya 'withholding' kwa kukata, kukusanya na baadaye kulipa Serikalini kodi itakayotozwa kwa mapato ya wateja yatokanayo na malipo ya riba. Viwango vinavyopendekezwa ni 10% kwa wenyeji (residents) na 15% kwa wageni. Inapendekezwa hatua hii ianze kutekelezwa tarehe 1 Julai, 1992. Jumla ya mapato yanavotarajiwa kwa hatua hii ni Sh. 1,000 milioni. Hatua hii haitawahusu wale wenye kupata mapato hayo ya riba yasiyozidi Sh. 150,000/- kwa mwaka.

(ii) Inapendekezwa pia kuwa kuanzia tarehe 1 Julai, 1992 kodi inayotozwa kwa gawio (dividends) zinazotangazwa (declared) na makampuni, zitozwe kodi mara moja tu (once and for all) wakati gawio linapolipwa baada ya hapo wenye hisa ambao watalipwa gawio hawatawajibika tena kulipia kodi mapato hayo. Kiwango kinachopendekezwa ni asilimia ishirini (20%). Hatua hii itailetea Serikali mapato ya ziada ya Sh. 34 milioni.

(iii) Hatua nyingine ya tatu kwa sheria hii ya Kodi ya Mapato ambayo itaiingizia Serikali mapato ni ile ya kuteremsha viwango vya kodi kwa walipakodi binafsi ambayo nimekwisha kuieleza awali ambayo inakwenda sambamba na hatua ya kuongeza mishahara ya watumishi. hatua hizi zitailetea Serikali mapato ya ziada ya Sh. 1,200 milioni.

75. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo Serikali inakusudia kuchukua inahusu kuongeza kodi ya ardhi (land rent). Hivyo sheria ya Ardhi (The Land Ordinance) inapendekezwa kufanyiwa mabadiliko mawili: moja ni kuongeza viwango vya sasa vya kodi ya ardhi (land rent) kwa asilimia ishirini (20%); na pili kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kuongeza thamani ya viwanja vya ardhi kwa wastani wa 33% katika makundi yafuatayo:—

(i) Viwanja vilivyokuwepo na vilivyotolewa kati ya tarehe 1 Julai, 1974 na 30 Juni, 1980 thamani yake iongezwe kwa asilimia hamsini (50%).

(ii) Viwanja vilivyopimwa na kutolewa kati ya tarehe 1 Julai, 1980 na 30 Juni, 1985 thamani yake iongezwe kwa asilimia thelathini (30%).

(iii) Viwanja vilivyotolewa kati ya tarehe 1 Julai, 1985 hadi 31 Desemba, 1991 thamani yake iongezwe kwa asilimia ishirini (20%).

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya mawili ambayo yatatekelezwa kwa pamoja imekadiriwa yataingizia Serikali mapato ya ziada ya Sh. 60 milioni. Hatua hizi zinapendekezwa kuanza tarehe 1 Julai, 1992.

76. Mheshimiwa Spika, hatua ya **saba** katika eneo hili la kodi inahusu sheria ya Usajili na Usihiaji wa Magari—The Motor Vehicles (Tax on Registration and Transfer) Act, 1972 pamoja na ile ya Road Traffic Act, 1973. Serikali inapendekeza kufuta nambari na usajili wa magari kwa kutumia herufi za **"TX"**. Usajili wa aina hii ulianzishwa miaka ya nyuma kwa sababu kuu mbili: moja ni kuwa Serikali ilitaka kudhibiti umilikaji na uuzaji wa magari hayo hasa kwa kuwa yalikuwa hayajalipiwa kodi na hivyo ingekuwa rahisi kuyafuatilia na kudhibiti ulipaji wa kodi iwapo yangeuzwa. Mheshimiwa Spika, sababu zote hizi mbili hivi sasa hazipo tena. Sheria ya vibali ilifutwa na Bunge lako tukufu mwanzoni mwa mwaka huu. Aidha

hivi sasa yapo magari mengi ambayo hayajalipiwa kodi lakini yana nambari za kawaida. Kwa mfano magari ya Watumishi wa umma ambao wamepewa nafuu ya 5%, au yale ya mashirika ya dini, na pia sasa yale ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, Serikali haioni sababu ya kuendeleza kuwa na usajili wa magari ya "TX". Tumeongeza matabaka ya nambari za usajili ambazo zinaleta utatanishi usio wa lazima. Kwa vile nambari hizo zitafutwa, itapasa magari hayo yote yasajiliwe upya na kodi ya usajili itapasa kulipwa. Kwa baadhi ya watu itapasa pia walipe kodi ya usihiaji (transfer) kwa sababu inafahamika kuwa wapo wenzetu wengi ambao walinunua na kutumia magari hayo lakini hawajafanya usihiaji. Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa itaiongezea Serikali mapato ya Sh. 28 milioni.

77. Mheshimiwa Spika, hatua hizi saba katika eneo la kodi inakadiriwa zitailetea Serikali jumla ya Sh. 4,004 milioni ambazo zitapunguza pengo la awali la Sh. 16,000 milioni kubakia na pengo la Sh. 11,996 milioni.

78. Mheshimiwa Spika, nilieleza hapo awali juu ya uamuzi wa Serikali kufuta misamaha mingi ya kodi ambayo imekuwepo, pamoja na hatua za kurekebisha baadhi ya misamaha mingine ili kuziba mianya iliyopo. Hatu hii imekadiriwa itaokoa mapato yasiyopungua Sh. 9,850 milioni. Kiasi hiki ni salio ambalo litabakia baada ya kuzingatia kuwa itapasa bajeti za Wizara mbali mbali pamoja na ruzuku kwa Serikali za Mitaa na baadhi ya Mashirika, zirekebishwe ili kuziwezesha kulipa kodi kama ilivyoamuliwa. Hivyo kiasi hicho Sh. 9,850 milioni kitapunguza pengo, na kubakiza pengo la Sh. 2,146 milioni ambalo itabidi kuzibwa kwa mapato mengine.

**Mapato yasiyo ya Kodi:**

79. Mheshimiwa Spika, eneo la pili la hatua hizo mpya linahusu kuongeza ada za huduma mbali mbali ambazo Serikali inatoa kwa jamii. Kwa hiyo Serikali inapendekeza kuongeza viwango vya ada zifuatazo:

(i) Ada zinazotozwa na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (Office of the Administrator-General) kwa ajili ya hati za kuzaliwa watoto, hati za vifo, hati za ndoa n.k.

(ii) Ada za leseni za Mafundi wa Umeme zinazotolewa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

(iii) Ada za huduma mbali mbali za Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

80. Mheshimiwa Spika, lengo la kuongeza viwango hivyo vya ada mbali mbali ni kuwa licha ya kutaka kuipatia Serikali mapato zaidi, hatua hii pia ni ya kurekebisha viwango hivyo vya ada ambavyo baadhi yake vimekuwa ni vidogo mno ukilinganisha na gharama halisi za kutoa huduma hizo. Baadhi ya viwango hivyo viliwekwa miaka ishirini au thelathini iliyopita. Vingine viliwekwa mwaka 1922. Aidha Serikali inataka wanaopata huduma hizo wachangie angalau kwa sehemu fulani gharama halisi ya utoaji huduma hizo. Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kuongeza ada mbali mbali imekadiriwa zitaingizia Serikali mapato ya ziada ya Sh. 338 milioni. Kiasi hicho kitapunguza pengo na kubakia Sh. 1,808 milioni.

**Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato:**

81. Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha Sh. 1,808 milioni kinategemewa kupatikana katika eneo la tatu la hatua mpya ambalo ni kuimarisha mbinu za kukusanya mapato. Mbinu hizo ziko katika maeneo matano.

Eneo la kwanza linahusu Kampuni za Ukaguzi wa Bidhaa (Pre-shipment Inspection Companies) ambazo zitakabidhiwa pia jukumu la kukadiria kiasi cha kodi wakati wa ukaguzi wa bidhaa zinazotoka nje. Lengo la hatua hii ni kupunguza urasimu na kusaidia kuondoa udanganyifu wa kukwepa kodi. Aidha hatua hii itarahisisha ulipaji wa mapato na hivyo inatarajiwa itaipatia Serikali mapato ya ziada.

82. Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni ya Idara za Kodi kutumia Mawakili Binafsi kudai kodi. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inao upungufu wa Mawakili na kesi nyingi za Serikali zikiwa ni pamoja na zile zinazohusu malipo na madai ya kodi hazimaliziki upesi. Serikali imeamua kuwa ili kuharakisha malipo ya maduhuli ya Serikali, Idara za Kodi ziruhusiwe kuwatumia mawakili binafsi kusaidia kesi zao ambao watalipwa kwa utaratibu uliopo kutegemea kiwango kitakachokusanywa. Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia sana kuharakisha malipo ya madeni ya kodi na mapato mengine. Kwa njia hii Serikali ina matumaini ya kuongeza mapato yake.

83. Mheshimiwa Spika, hatua ya **tatu**, ya kuimarisha mbinu za ukusanyaji mapato inahusu ukusanyaji wa mapato yatokanayo na 'import support' wanazopewa watu na mashirika mbali mbali. Imedhihirika kuwa baadhi ya watu wanaopewa fedha hizo huwa wanachukua muda mrefu kulipa fedha hizo Serikalini. Mheshimiwa Spika, ili kuwabana watu hao, Serikali inapendekeza kiwepo kipengele cha sheria ambacho kitawalazimisha kulipa madeni hayo kwa wakati unaotakiwa na wakishindwa hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia sana kuongeza mapato.

84. Mheshimiwa Spika, hatua ya **nne**, ni ya kuwataka wale wote wanaoruhusiwa kulipa kodi kwa awamu (instalments) sasa wapewe muda usiozidi miezi kumi na miwili (12). Aidha malipo hayo ya awamu sasa yatakuwa yanatozwa riba kwa kiwango kilicho sawa na kile ambacho Serikali yenyewe hulipa Benki Kuu kwa mikopo yake. Hatua hii itawafanya wale walipakodi ambao wana tabia ya kuzembea kulipa kulazimika kulipa kwa wakati wake vinginevyo watalipa kodi zaidi kwa sababu ya kulipa riba.

85. Mheshimiwa Spika, eneo la tano la kuimarisha ukusanyaji wa mapato litahusu kuundwa upya kwa Idara ya Forodha na Kodi ya Mauzo siyo tu kwa ajili ya kutaka kuleta ufanisi wa utendaji, bali pia kwa ajili ya kujiandaa na mfumo mpya wa kodi ya mauzo inayofuata ongezeko la thamani (Value-Added Tax—VAT) badala ya kodi ya mauzo ya sasa. Mfumo huo mpya utaanza kutumika Januari 1994. Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la kuimarisha ukusanyaji wa mapato hatua pia zinakusudiwa kuchukuliwa ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa) zinashauriana juu ya suala hili kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuimarisha ukusanyaji mapato kwa ajili ya Serikali za Mitaa katika vianzio vya kodi ambazo Serikali Kuu imeachia.

86. Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kiutawala za kuimarisha makusanyo, zinatarajiwa zitaingizia Serikali kiasi kisichopungua hizo Sh. 1,808 milioni ambazo zitatosheleza kuziba pengo hilo la mapato.

**Masuala mengine muhimu:**

87. Mheshimiwa Spika, mbali na hizo hatua mbali mbali za kuziba pengo ningependa pia kulieleza Bunge lako tukufu juu ya maamuzi na hatua nyingine ambazo Serikali itazichukua kwa mwaka wa fedha ujao wa 1992/93. **Kwanza** ni kuwa kuanzia tarehe 1 Julai, 1992 ule utaratibu wa sasa wa kuoanisha bidhaa (tariff clasification of goods) utabadilishwa. Badala ya kutumia mtindo wa "Customs Cooperation Council Nomenclature" au kwa kifupi "CCCN", sasa utaachwa na tutaanza kutumia "Harmonised Commodity Description and Coding System" au kwa kifupi "HS" ambao ndiyo unatumiwa siku hizi na mataifa mbali mbali, ikiwa ni pamoja na nchi jirani kama vile Kenya, Zambia, Malawi na Zimbabwe. Maandalizi ya kwanza kutumia utaratibu huu mpya yamekamilika.

88. Mheshimiwa Spika, sambamba na kuanza kutumia utaratibu wa "HS" vile vile kwa makubaliano na wenzetu katika PTA, tunatakiwa kuchapisha na kutangaza "PTA Tariff" ambayo itaanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 1992. "Tariff" hiyo ambayo tayari ni "harmonised system" nayo matayarisho yake yamefikia kiwango kikubwa cha utekelezaji.

89. Mheshimiwa Spika, suala la mwisho linahusu kuanzishwa kwa mifuko mipya. Mfuko wa **kwanza** ambao Serikali inakusudia uanzishwe ni ule utakaoitwa Mfuko wa Maendeleo ya Utalii (The Tourism Development Fund). Mfuko huu ulifutwa huko nyuma mwaka 1985, lakini kwa kuzingatia umuhimu wa kutaka kuendeleza shughuli za utalii kwa siku zijazo, Serikali imeamua kuanzisha mfuko huo. Inatarajiwa mfuko huo utaanza kwa kuwa na Sh. 600 milioni ambazo zitatokana na sehemu ya mapato ya kodi ya hoteli (Hotel Levy) inayokusanywa na Serikali Kuu.

90. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa **pili** unaokusudiwa kuanzishwa mwaka ujao wa 1992/93 ni Mfuko wa Kukopesha wanafunzi (Education Loan Fund). Maaudalizi ya kuanzisha Mfuko huu bado yanakamilishwa, na mara yatakapokuwa tayari, Serikali italeta mapendekezo yake ili Bunge likikubali lipitishe Azimio linalohusika.

91. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa **tatu** ni ule wa "Road Fund". Mfuko huu ulianzishwa mwaka jana kwa ajili ya matengenezo na uangalizi (maintenance) ya barabara chini ya IRP. Mfuko huo hupata fedha zake kutokana na ushuru wa barabara (Road Toll). Serikali inapendekeza Mfuko huo utunishwe ili uwe na kiasi cha Sh. 7,000 milioni. Fedha za nyongeza hiyo zitatokana na ongezeko la kiwango cha "road toll" hiyo ambacho sasa kitakuwa Sh. 10/- kwa kila lita ya dizeli na petroli, badala ya Sh. 7/- za sasa.

92. Mheshimiwa Spika, baada ya kutangaza hatua hizo mpya za mapato zinazopendekezwa, napenda kutoa muhtasari wake, pamoja na mapato ya ziada yanayotarajiwa kama ifuatavyo:—

| | | Sh. |
|---|---|---|
| (i) | Kodi ya Uwanja wa Ndege .... | 72 milioni |
| (ii) | Kodi ya kusafiri katika Meli .. | 5 milioni |
| (iii) | Kodi ya Mapato: | |
| | (a) Kodi kwa riba zinazotokana na akiba za Benki | 1,000 milioni |
| | (b) Kodi kwa mishahara mipya | 1,200 milioni |
| | (c) Kodi ya 20% kwa gawio . | 34 milioni |
| (iv) | Kodi ya Ardhi ........................ | 60 milioni |
| (v) | Ushuru wa Barabara ............ | 1,353 milioni |
| (vi) | Uandikishaji upya wa Magari ya TX ................................ | 28 milioni |
| (vii) | Ushuru kwa Lubricant kutoka nje | 252 milioni |
| (viii) | Ongezeko la Ada mbali mbali | 338 milioni |
| (ix) | Kuondolewa kwa Misamaha ya Kodi ................................ | 9,850 milioni |
| (x) | Hatua za kuimarisha ukusanyaji mapato ...................... | 1,808 milioni |
| | Jumla ... | 16,000 milioni |

**SURA YA BAJETI YA MWAKA 1992/93**

93. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kuhusu mbinu mbali mbali za kupata mapato mapya ya kukidhi mahitaji, sura ya bajeti ya mwaka 1992/93 inajitokeza kama ifuatavyo:—

| | Sh. |
|---|---|
| Matumizi ya kawaida ..... | 251,543 milioni |
| Matumizi ya maendeleo . | **102,062** milioni |
| Jumla ya Matumizi ......... | **353,605** milioni |
| Mapato ya kawaida ......... | 215,607 milioni |
| Mikopo na Misaada ya Nje | 140,998 milioni |
| Mikopo isiyo na Mabenki | 7,000 milioni |
| Mikopo ya Mabenki ........ | **(10,000)** milioni |
| Jumla ya Mapato ............ | **353,605** milioni |

Hivyo Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza sura hii ya bajeti kwa Bunge lako tukufu kwa mwaka 1992/83.

**MWISHO**

94. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa mapato ya wananchi yameendelea kuwa ni madogo na hivyo mapato ya Serikali kutokana na kodi pia yamekuwa madogo. Wakati huo huo matumizi ya Serikali yameendelea kuwa makubwa kuliko mapato na hivyo kuhitaji kiwango kikubwa cha misaada na mikopo kutoka kwa wahisani wa nje. Katika mwaka 1991/92, mchango wa moja kwa moja wa wahisani katika kugharamia matumizi ya Serikali utafikia asilimia 30. Mchango huo ni mkubwa zaidi ikizingatiwa kwamba mbali na mchango wa moja kwa moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kuna pia misaada ya uagizaji (Import Support), pamoja na kiasi kikubwa cha misaada ya kutuongezea uwezo kwa upande wa mizania ya malipo na nchi za nje (Balance of Payments Support).

95. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba kuendelea na bajeti ya namna hiyo ni sawa na Serikali kuwabebesha wananchi mzigo ambao hawana uwezo nao. Hivyo Serikali sasa haina budi kuchukua hatua madhubuti kuirekebisha hali hiyo, ili matumizi ya Serikali yalingane na mapato yake. Inabidi kama walivyohusia Wahenga, tushone koti letu kulingana na kitambaa kilichopo. Ili kufikia lengo hilo Serikali haitaweza kukwepa kuangalia upya majukumu yake, kwa madhumuni ya kujitoa katika yale maeneo ambayo yanaweza kufanywa vizuri zaidi na vyombo vingine. Kadhalika, kwa zile shughuli ambazo zitaendelea kusimamiwa na Serikali, kama huduma za jamii, wananchi nao itabidi wachangie katika ujenzi na uendeshaji wake ili kuipa uwezo Serikali wa kutoa pamoja na kuzipanua huduma hizo.

96. Mheshimiwa Spika, nimekwisha eleza hapo awali mabadiliko ya muundo na viwango vya kodi mbali mbali. Shabaha kubwa ya mabadiliko hayo ni kutoa changamoto (challenge) mpya kwa wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara wa nchi hii, pamoja na marafiki wa Tanzania walioko nje ya mipaka yetu. Tegemeo la kwanza ni kwamba kodi zote zinazotakiwa kulipwa zitalipwa kwa wakati. Serikali haina miujiza ya aina nyingine yoyote ya kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi wake isipokuwa kwa wananchi hao kuipa uwezo Serikali yao kwa kulipa kodi zinazotakiwa. Hivyo kipimo cha kwanza cha raia mwema ni kulipa kodi zake kwa wakati, kwani bila ya kodi hakuna maendeleo. Haina maana kuendesha magari mazuri katika barabara ambazo magari hayo yanapita kwa shida kwa sababu ni mbaya sana kutokana na kukosa matengenezo yanayosababishwa na ukosefu wa fedha. Hatuna budi kujenga utamaduni wa kulipa kodi zetu mapema na sheria zitawabana wakwepaji bila ya huruma wala upendeleo.

97. Mheshimiwa Spika, tegemeo la pili ni kwamba wafanyabiashara na wawekezaji rasilimali kwa jumla, sasa hawana sababu kabisa ya kuendesha shughuli zao kwa kificho. Nawaomba wajenge tabia ya kufanya shughuli zao katika mikondo rasmi na iliyo bayana. Serikali haina nia ya kuchukua kutoka kwao zaidi ya zile kodi nafuu kabisa zilizotangazwa leo hii, kwa ajili ya kufanyia kazi zenye manufaa kwetu wote. Sina haja ya kusisitiza zaidi kwamba sera sahihi za maendeleo ya uchumi wa Taifa letu, zinategemea sana kuwepo kwa tathmini sahihi ya hali ilivyokuwa katika kipindi kilichopita pamoja na malegemeo yasiyotiwa chumvi kwa kipindi kinachofuata. Yote haya hayawezekani bila ya kuwepo "data" na takwimu sahihi kuhusiana na shughuli mbali mbali za Taifa. Kwa mfano, kuna hisia kwamba biashara inayofanyika kati ya nchi yetu na nchi za nje ni kubwa, karibu mara dufu, kuliko takwimu zetu za kila mwaka za mauzo na uagizaji kutoka nje zinavyoonyesha. Huu ni udhaifu mkubwa kwani bila ya kuwa na takwimu sahihi za mauzo na ununuzi kutoka nje, hatuwezi kuwa na sera sahihi kuhusu thamani ya fedha yetu (exchange rate policy) na matokeo yake ni kutokuwa na uchumi uliotengemaa. Hivyo baada ya Serikali kutekeleza ahadi zake kwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya fedha, mashirika ya umma, udhibiti wa fedha za kigeni, pamoja na kodi mbali mbali, linalobaki sasa ni kwa wafanyabiashara wetu na wawekezaji rasilimali, kwa jumla, nao kutekeleza ahadi yao kwa Taifa hili, nayo ni kuongeza na kupanua viwango vya shughuli zao, kulipa kodi kwa wakati, na kutoa takwimu sahihi kwa vyombo vinavyohusika. Kadhalika ni mategemeo ya Serikali pia kwamba nafuu mbali mbali zilizotolewa katika bajeti hii zitamfikia pia mlaji wa kawaida, kwa kupunguza bei za bidhaa na huduma wanazozitoa.

98. Mheshimiwa Spika, tegemeo la tatu ni kwamba watumishi wetu wa Idara za Mapato nao wataongeza juhudi na ufanisi katika kukusanya mapato ya Serikali.

Huko nyuma pamoja na matatizo ya vitendea kazi na marupurupu duni, watumishi hao wamekuwa wakifanya kazi nzuri, ingawa pamekuwa na watumishi wachache ambao wamekuwa wakichafua jina zuri la Idara zetu hizo. Katika mwaka 1991/92, kwa mfano, Idara hizo zinatarajiwa kukusanya mapato kutokana na kodi ya Sh. 158,389 milioni, ambazo ni sawa na asilimia 18 zaidi ya viwango vya mapato ya kawaida ya Serikali yaliyoidhinishwa na Bunge ya Sh. 134,094 milioni. Ninaamini kabisa kwamba kwa kuwaondolea baadhi ya matatizo yao, ambayo yako ndani ya uwezo wetu, Idara hizo zinaweza kukusanya zaidi kabisa ya kiwango hicho. Hivyo kuanzia mwaka 1992/93, kama nilivyokwisha sema, Idara hizo zikikusanya mapato zaidi ya viwango vilivyowekwa na Bunge hili, watapewa asilimia 20 ya mapato ya ziada kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wao bonasi pamoja na kujinunulia vitendea kazi. Mgawanyo kati ya kiwango cha bonasi na kile cha kununulia vitendea kazi utaamuliwa na Wakuu wa Idara zinazohusika kwa kushauriana na Katibu Mkuu wa Hazina. Ni dhahiri kadri Idara hizo zitakavyoweza kukusanya mapato zaidi ya ziada, ndivyo watakavyoweza kuwalipa wafanyakazi wao malipo makubwa ya bonasi, pamoja na kujiimarisha kwa vitendea kazi.

99. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hatua za kuimarisha mapato ya Serikali peke yake, bila ya wakati huo huo kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti matumizi ya Serikali, ni sawa na kujaza maji katika pakacha, kamwe haliwezi kujaa kwa sababu ya kuvuja. Hatua kadhaa nilizozieleza hapo awali zina lengo la kuimarisha mbinu mbali mbali za kudhibiti matumizi pamoja na kuzuia au hata kupunguza kasi ya kupanuka na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali. Kwa hiyo, marekebisho ya muundo na shughuli za Serikali, sekta ya fedha pamoja na mashirika ya umma, kwa jumla yana lengo la kudhibiti kupanuka kwa matumizi ya Serikali. Hii inatokana na ukweli kwamba mapato na matumizi


ya Serikali, ni kama pande mbili za sarafu ile ile, na hivyo hakuna upande unaozidi mwingine katika umuhimu wake. Kutokana na hali hiyo msukumo wa utekelezaji ni lazima uweke uzito sawa kwa pande hizo mbili.

100. Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni hatua muhimu katika kutekeleza sera za kiuchumi na kijamii ambazo tumejiwekea katika mipango yetu ya kufufua uchumi. Ni dhahiri yale ambayo tuna uwezo nayo tuyatekeleze na tufanye hivyo bila kuchelewa. Pale ambapo Serikali inaamua kuwekeza rasilimali yake, tuhakikishe kuwa matunda yanapatikana. Kadhalika, inabidi tuhusishe zaidi nguvu ya wananchi katika kuzalisha mali na kutoa huduma kwa kuwahamasisha kufanya kazi kwa bidii zaidi pamoja na kuweka vitega uchumi katika kilimo, viwanda, biashara, utalii na kwingineko. Hayo yote yamo katika uwezo wetu wa kuyatekeleza. Hatuna sababu ya kungoja kwani wakati ni mali pia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho A

## MSINGI WA BAJETI UKILINGANISHWA NA UWEZO (Mtsh) 1991/92




KULINGANA NA MAKUBALIANO YA 1986NA WAHASANI NIKWAMBA MISAADA NA MIKOPO YA KIASI HICHO ILITAKIWA KUWA YA MUDA WAKATI TUNATAFUTA NJIA ZA KUONGEZA MAPATO NA KUPUNGUZA MATUMIZI ILI KUPUNGUZA TEGEMEZI

Chanzo: Wizara ya Fedha

## MWENENDO WA BIDHAA YA VIGEZO MUHIMU VYA BIASHARA YA NJE

Jedwali Na. 1 (US $ milioni)

| Mwaka | 1981/82 | 1982/83 | 1983/84 | 1984/85 | 1985/86 | 1986/87 | 1987/88 | 1988/89 | 1989/90 | 1990/91 | 1991/92* | 1992/93** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Mauzo ya Bidhaa nchi za Nje ... | 570 | 369 | 347 | 335 | 317 | 355 | 362 | 393.90 | 424.50 | 393.6 | 422.4 | 600.0 |
| 2. Uagizaji kutoka Nje ... | 1,079 | 902 | 875 | 950 | 1,024 | 1,155 | 1,185 | 1,277.40 | 1,380.00 | 1,381.3 | 1,437.4 | 1,600.0 |
| 3. Urari wa Biashara ya Bidhaa ... | 509 | −533 | −528 | −615 | −707 | −800 | −823 | −883.5 | −955.5 | −987.7 | −1,012.0 | −1,000.00 |
| 4. Urari wa Biashara ya Bidhaa kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za Nje . | 89.3 | 114.2 | 112.2 | 184 | 223 | 225.4 | 227.3 | 224.3 | 225.1 | 250.9 | 239.6 | 166.7 |
| 5. Uagizaji Mafuta ya Petroli ... | 226 | 210 | 233 | 237 | 196 | 168 | 160 | 180.00 | 180.00 | 245.9 | 180.91 | 200.0 |
| 6. Uagizaji wa Mafuta ya Petroli kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za Nje . | 40 | 57 | 67 | 71 | 62 | 47 | 44 | 46 | 42 | 63 | 43 | 33 |

* Matarajio **** Makadirio.

*Chanzo:* Tume ya Mipango.

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA YA SERIKALI

Jedwali Na. 2

(Sh. Million)


| Mwaka | 1981/82 | 1982/83 | 1983/84 | 1984/85 | 1985/86 | 1986/87 | 1987/88 | 1988/89 | 1989/90 | 1990/91 | 1991/92* | 1992/93** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Kawaida ....... | 9,977.3 | 10,600.0 | 15,465.1 | 18,000.0 | 22,321.0 | 31,096.0 | 46,829.0 | 71,789.0 | 94,654.0 | 135,920.0 | 176,613.0 | 215,607 |
| Matumizi ya Kawaida .... | 13,213.9 | 14,589.3 | 18,182.0 | 20,674.0 | 27,403.0 | 38,774.0 | 61,765.0 | 92,652.1 | 115,893 | 160,3045 | 194,347.0 | 251,543 |
| Salio la Bajeti ya Kawaida ......... | -3,236.6 | -3987.3 | -2,716.4 | -2,674 | -5,082.0 | -7,678 | -14,936 | -20,773.1 | -21,238.2 | -24,973.2 | -17,734 | -35,936 |
| Salio % ya Matumizi ya Kawaida ......... | 24. | 13.6 | 14.9 | 12.9 | 18.5 | 19.8 | 24.2 | 22.4 | 18.3 | 15.6 | 9.1 | 14.3 |

* Matarajio.
** Makadirio.
Chanzo: Wizara ya Fedha.

*Jedwali Na. 3*

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

(Kwa mwaka unaoishia Juni ) (sh. Millioni)




Chanzo: Wizara ya Fedha

## MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA (TANI ZA METRIKI)

Jedwali Na. 4

| | 1981/82 | 1982/83 | 1983/84 | 1984/85 | 1985/86 | 1986/87 | 1987/88 | 1988/89 | 1989/90 | 1990/91 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkonge | 60,635 | 46,187 | 38,255 | 32,247 | 30,151 | 33,170 | 33,268 | 32,265 | 33,743 | 36,001 |
| Kahawa | 50,790 | 53,368 | 49,608 | 49,080 | 55,147 | 58,737 | 48,612 | 55,130 | 59,996 | 44,123 |
| Pamba | 132,926 | 127,910 | 140,798 | 154,865 | 105,367 | 214,569 | 254,915 | 188,395 | 112,905 | 149,141 |
| Tumbaku | 16,234 | 13,635 | 11,012 | 13,315 | 12,549 | 12,921 | 12,866 | 11,517 | 11,063 | 18,364 |
| Pareto | 1,807 | 1,601 | 1,438 | 1,533 | 1,352 | 1,231 | 1,412 | 1,313 | 1,242 | 1,672 |
| Majani ya Chai | 74,563 | 84,240 | 72,230 | 77,230 | 71,472 | 64,694 | 63,632 | 71,068 | 92,876 | 83,223 |
| Korosho | 44,331 | 32,966 | 48,306 | 32,532 | 18,901 | 16,548 | 24,287 | 19,275 | 17,059 | 28,870 |

Chanzo—KILIMO